**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents | Government Budget Speeches

1979-09-01

# Hotuba ya Rais Mwalimu Julius K. Nyerere aliyotoa siku ya mashujaa 1979

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/667

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MAPAMBANO YANAENDELEA

## Hotuba ya Rais Mwalimu Julius K. Nyerere Aliyoitoa siku ya Mashujaa

## Septemba 1, 1979

1979
KIMETOLEWA NA IDARA YA HABARI,
WIZARA YA HABARI NA UTANGAZAJI,
S.L.P. 9142, DAR ES SALAAM



Rais Mwalimu Julius K. Nyerere

# MAPAMBANO YANAENDELEA

## Hotuba ya Rais Mwalimu Julius K. Nyerere Aliyoitoa siku ya Mashujaa

Septemba 1, 1979

# MAPAMBANO YANAENDELEA

Ndugu Wananchi,

Leo ni siku ya Mashujaa. Siku hii kila mwaka tunawakumbuka mashujaa wetu waliojitoa kupigana na wavamizi kutoka katika nchi za nje au wageni waliotaka kuitawala nchi yetu. Tunawakumbuka, kwa heshima, wale waliopigana kuwazuia Wakoloni wasiitawale Tanzania, na wale waliopigana katika vita vya Maji Maji katika jitihada za kupinga utawala wa Kijerumani. Wachache wao tunawafahamu, na majina yao tunayaheshimu: mashujaa kama Mkwawa, Mirambo, na Mputa. Lakini wengi wao hatuwafahamu kwa majina; ila tunafahamu tu ya kwamba walipigana, na kufa, katika jitihada za kutetea uhuru wa nchi yetu. Tunawakumbuka na kuwaheshimu.

Leo tena tunawakumbuka mashujaa hao kwa fahari. Juhudi zao na vitendo vyao vilitutia moyo siku za nyuma na vinatutia moyo mpaka sasa. Hatutawasahau.

Lakini siku ya mashujaa ya leo ni siku maalum. Miezi kumi iliyopita nchi yetu ilivamiwa na majeshi ya Idi Amin. Majeshi hayo yakachukua sehemu ya ardhi yetu, na Amin akatangaza kwa jeuri kabisa kuwa amebadili mipaka. Akadai kwamba kuanzia siku hiyo sehemu yote ya Missenyi itakuwa ni sehemu ya Uganda. Na akatishia kuchukua sehemu kubwa zaidi ya Tanzania. Wananchi wote wa Tanzania walichukizwa sana na kitendo hicho. Tukajua kwamba kila mmoja wetu anataka adui huyo afukuzwe nje ya mipaka yetu na aadhibiwe. Wananchi kwa nia moja wakawa radhi kabisa kujitoa mhanga na kukubali shida zo zote zitakazotokea kwa sababu ya kumwadhibu mvamizi huyu. Hakuna aliyesita au kurudi nyuma. Wananchi vijijini na mijini walitoa walichokuwa nacho kusaidia vita. Walichanga ng'ombe, mahindi, maharage, fedha na wakaongeza sana juhudi ya kazi. Maelfu walichanga damu.

Na wote wakakubali bila ya manung'uniko upungufu wo wote wa huduma za kawaida, ilipokuwa lazima kutumia huduma hizo kusafirisha askari, silaha, chakula na vifaa vingine kupeleka vitani.

Bila ya moyo na mwitikio huo, tusingeweza kupigana na kushinda vita. Maana vita vya siku hizi havipiganwi na askari peke yao; vita vya kisasa vinawashirikisha watu wote. Kwa kila askari aliye katika mstari wa mbele, lazima waweko askari wengine wengi huku nyuma wakisimamia usafirishaji, wakipeleka na kupokea habari, na wakipanga mbinu za mashambulizi. Na kwa kila askari, popote alipo, lazima waweko raia kwa mamia wanaojishughulisha na kutengeneza viatu na nguo za askari, na chakula cha wapiganaji, na vile vile kupakua silaha kutoka katika meli au ndege, na kuhakikisha kwamba usafiri wa reli, wa barabara na wa ndege unaendelea kwa ufanisi kadiri inavyowezekana.

Wala si askari peke yao wanaoumia au kufa. Raia wengine, ingawa kwa bahati nzuri si wengi, waliuawa au kujeruhiwa wakati ndege za Amin zilipoangusha mabomu Bukoba na Mwanza. Na maelfu ya wananchi waliokuwa wakiishi katika eneo Amin aliloliteka ama wameuawa ama wamejeruhiwa vibaya sana. Hata wale walionusurika walipoteza vyote walivyokuwanavyo: nyumba zao, na vitu vichache walivyokuwanavyo; shule zao, zahanati zao, na mashamba yao!

Katika siku hii ya leo tunakumbuka juhudi zetu na shida tulizozipata. Na hasa tungependa kukumbuka ujasiri wa raia waliokuwa wanaishi karibu na mpaka, ambao waliteseka kwa uvamizi wa Amin, lakini ambao walisimama imara wakaendelea na kazi zao za kilimo na za kuendeleza huduma za lazima.

Lakini katika vita, hata kama sisi sote tunahusika, bado kazi ya askari ni kazi maalum. Wao ndio huenda mbele kumkabili adui. Wao ndio makusudi kabisa huyaweka maisha yao katika hatari kubwa. Wanakwenda wakati wowote, na mahali po pote wanapoamriwa kwenda, bila ya kujali shida zitakazowakabili katika kwenda hivyo; au muda waliokwisha kuutumia katika kupigana au

kutembea. Giza likiingia wanalala hapo hapo walipo (na katika vita hivi wamewahi kulala sehemu za maji na mbu na majoka), lakini walinzi wa doria wakati wote lazima wawe tayari kupambana na adui mara tu zitokeapo dalili za kwanza za hatari.

Na katika vita hivi vya kupambana na Amin, baadaye askari wetu walilazimika kuvuka mpaka wa Tanzania na kuingia katika nchi ambayo si yao. Walilazimika kufanya hivyo ili kumwadhibu mvamizi, na kuhakikisha kwamba hana uwezo tena wa kurudia mashambulizi yake katika nchi yetu. Haikuwa kazi rahisi. Hawakuwa na hakika kuwa watapokewa kwa shangwe na wananchi wa Uganda ambao walikuwa wamechoshwa na ukatili wa Amin. Lakini walivuka mpaka; na wakamwadhibu Amin.

Na wamemwadhibu kweli! Urais wa maisha ukomile, na kujigamba kukomile! Amin sasa ni mkimbizi katika nchi alikozoea kwenda kifua mbele akijitapa juu ya ujasiri wake.

Tanzania haina jeshi kubwa; ila ina jeshi zuri. Lakini Tanzania ina wananchi wengi ambao ni wanamgambo. Jeshi la Wananchi pamoja na wanamgambo waliungana kuunda nguvu moja ya mapigano. Nguvu hiyo ya pamoja ndiyo iliyompiga Idi Amin. Siasa yetu ya kuwafunza ulinzi wananchi wa vijijini, viwandani, maofisini, na kulifanya Jeshi la Wananchi kusimamia mafunzo hayo, imethibitika kuwa siasa safi. Tunawapa heko. Tunampongeza kila askari ambaye alitimiza jukumu lake kwa uaminifu na kwa nidhamu: aliyekuwa vitani Uganda na aliyekuwa huku nyuma.

Baadhi yao wapo pamoja nasi hapa leo. Tunawakaribisha na kuwapokea. Tunawapokea kwa niaba yao wenyewe, na pia wakiwa wawakilishi wa wenzao waliokwisha kwenda nyumbani katika sehemu mbali mbali za Tanzania, na pia wale ambao wako Uganda bado.

Kama mlivyokwisha kutangaziwa, majeshi yetu yameanza kurudi nyumbani. Kiasi cha elfu ishirini, karibu nusu ya wapiganaji wote waliokuwa Uganda, wamekwisha kurudi makwao. Wale ambao bado wako Uganda watarudi mara

matayarisho yatakapokamilika ya kuondoka kwao Uganda bila kuacha fedheha. Hawa ni vijana wetu. Tunataka warudi nyumbani wawe pamoja nasi. Tunahitaji juhudi zao na moyo wao katika kujenga nchi yetu.

Lakini wako baadhi ya askari wetu ambao hawatarudi tena. Vijana wetu 404 wamekufa vitani. Tunawapa heshima zetu, kwa huzuni lakini pia kwa fahari. Tunatoa pole nyingi kwa jamaa zao, na tunaungana nao katika msiba huo. Shida yao ni shida yetu, na maisha yao ya siku za mbele ni jukumu letu.

Na baadhi ya askari wetu walijeruhiwa. Wengi wao wamepona, au watapona kutokana na matibabu tunayowajibika kuwapa. Lakini baadhi yao wamepata vilema vya maisha. Kwao hao tunao wajibu maalum. Ni wajibu wa Chama, wa Serikali na wa kila mwananchi, kuwasaidia waweze kuwa raia wenye manufaa kwa kiasi cha uwezo wa hali yao. Maana mtu haachi kuwa na manufaa kwa sababu tu amekatika mguu, au mkono, au amepoteza macho yake, au amevurugika akili. Inawezekana kazi fulani hataweza kuzifanya, lakini ziko nyingine anazoweza kuzifanya. Hatuna budi kuhakikisha kuwa hawa walioumizwa kutokana na uvamizi wa Amin, hawa ambao walipigana kwa ajili yetu sisi wote, wanapata mafunzo mapya pale ambapo inawezekana, halafu wanapata nafasi ya kujipatia riziki zao katika kazi ambazo wanaziweza. Kila mtu mwenye jukumu la kuwaajiri wafanya kazi lazima akumbuke wajibu huo. Na kila mfanya kazi lazima awasaidie askari hawa walemavu kufanya kazi zao na kutimiza wajibu wao kwa ukamilifu katika maisha yetu.

**Vita vyenyewe**

Juu ya vita hakuna mengi ya kusema. Kama mnavyokumbuka vita vilianza kwa jeshi la Tanzania kurudishwa nyuma. Hilo halikuwa jambo la ajabu, wala si jambio la kuona aibu. Hatukuwa tumejiandaa kupigana vita, na wala hatukuwa na askari wengi mpakani. Mtu anayeshambulia bila ya kuchokozwa siku zote hupata nafasi nzuri pale mwanzo. Lakini jambo kubwa si mwanzo; jambo kubwa zaidi ni mwisho. Anayecheka jioni huzidiwa asubuhi. Sisi tulijibu kwa kujiwekea mipango na matayarisho

mazuri. Najua kuwa watu fulani hata baadhi ya Watanzania walidhani kuwa tulikuwa hatufanyi kitu. Amin alikuwa akijitapa kwa makelele mengi juu ya ushindi wake, na sisi tulikuwa hatusemi mengi. Adui alikaa katika sehemu ya Missenyi kwa majuma mengi. Amin alitunga uwongo kuwa sisi tulikuwa tunamshambulia ili aweze kutamba kuwa alikuwa anaturudisha nyuma. Lakini hakukuwako mashambulizi, isipokuwa ya mizinga kidogo tu. Na baadhi yenu pia mlidanganyika. Mkaanza kuuliza, "Mwalimu ameanza mambo yake ya siasa tena, au Jeshi letu halina uwezo wa kufanya lo lote?"

Tulipanga mashambulizi yetu kwa uangalifu sana, na tukasafirisha vilivyohitajiwa katika mashambulizi yale kabla ya kufanya jambo lolote kubwa. Tulikuwa na shabaha mbili. Kwanza, kushinda vita. Pili, kushinda vita bila kupoteza askari wengi mno. Maisha ya kila Mtanzania ni ya thamani kubwa. Hatuwezi kupoteza maisha bure ili tuweze kujigamba tu kuwa sisi ni hodari.

Basi tuliuvuka mto. Halafu tukatembea kwa miguu kusonga mbele. Askari wetu ni askari wa miguu; mwendo wote walitembea kwa miguu. Tulisonga mbele taratibu na kwa mpango. Mara moja tulielemewa. Kijiji kimoja kidogo tulikichukua na kikachukuliwa tena na maadui mara nyingi; na mara moja, tulitumbukia katika mtego. Lakini hatukubabaika na hata mara moja hatukufa moyo. Vikosi vilijipanga upya na kusonga mbele tena. Na wakati wote walishirikiana na Jeshi la Ukombozi la Uganda. Viongozi wa Jeshi la Uganda Ndugu Okello na Ndugu Ojok, walio hapa leo pamoja nasi.

Majeshi hayo ya ukombozi, katika mapigano ya pamoja: yaliingia Kampala. Na baada ya hapo, kwa kuombwa na serikali mpya ya Uganda, wakaendelea kusonga mbele na kupigana katika Uganda nzima, kufagiafagia mabaki ya majeshi ya Amin, na kuuzia uwezekano wo wote wa majeshi hayo kurudi tena.

Sasa vijana wetu wanarudi. Na mashujaa tunaowapa heshima leo ni vijana hao wa jeshi letu **la Ulinzi**. Hawa si sehemu, na wala hawana haja ya kuwa sehemu, ya jeshi la uvamizi. Wale walioko Uganda hivi sasa wako huko kwa

kuombwa na Serikali ya Uganda, wakati Serikali hiyo inaandaa mipango mingine ya ulinzi wa Uganda. Mara mipango hiyo itakapokamilika na tumeitaka serikali ya Uganda ifanye haraka katika jambo hilo, vijana wetu watarudi.

Lakini napenda kueleza wazi kwamba, kwa sasa uongo na visingizio vinavyoelezwa juu ya majeshi ya Tanzania katika Uganda havitatuzuia sisi kutimiza wajibu wetu. Anapotokea askari mmoja mmoja amefanya vitendo vya utovu wa nidhamu, basi askari huyo atachukuliwa hatua kali na kwa haraka. Lakini hatutatumbukia katika mtego wa kutomwamini askari wetu yeyote kwa sababu ya visingizio vya wenye hila.

Maana uongo huu unaoenezwa ni sehemu ya mapambano ya kisiasa ya kuipinga Tanzania na Serikali mpya ya Uganda. Wale wanaoeneza uongo huo wanazo sababu zao wenyewe. Lakini si sababu za kweli, wala si za heshima. Uongo huu unatoka kwa watu ambao walinyamaza kimya kwa muda wote wa miaka minane ya utawala wa kikatili wa Idi Amin. Baadhi ya watu wanaoeneza uongo huu walikula na Amin, walikunywa na Amin, waliiba na Amin na waliua na Amin. Ushindi wa majeshi yetu umewaondolea uhondo wao. Baadhi yao ni wale waliodhani kuwa zamu yao ya kuwaibia na kuwanyonya Waganda imefika. Ushindi wa majeshi yetu, umewaondolea matumaini yao. Walianza uongo wao mara matumaini yao yalipofutwa na msimamo wa wananchi wa Uganda wanaodai umoja, wanaotaka nafasi ya kujenga upya uchumi wa nchi yao, na wanaotaka kuipa nchi yao Serikali inayojali shida za wananchi wa Uganda. Sasa waongo hao wanaeneza uvumi na kashfa ambazo ni kinyume kabisa cha msimamo na shabaha za wazalendo wa Uganda.

Watu hao wanaweza wakawa na vyeo vikubwa katika nchi zao; wanaweza wakawa na shahada za kisomo cha hali ya juu; wanaweza wakawa matajiri wa fedha; wanaweza wakavuruga mawazo ya wananchi wachache wasiokuwa na hatia. Lakini ni watu takataka; hawastahili hata kutemewa mate. Lakini wanasema; acha waseme.

Majeshi ya Tanzania yalipokelewa na wananchi wa Uganda kwa shangwe, na wananchi wa Uganda wakatumia kuwapo kwa majeshi yetu kuuangusha utawala wa kikatili wa Idi Amin. Majeshi ya Tanzania yaliingia Uganda kwa heshima; na wanarudi kwa heshima zaidi: Tunajivunia vijana hawa; na tunawapongeza.

**Baada ya Vita**

Vita sasa vimekwisha. Lakini kusema hivyo maana yake si kusema kuwa tunaweza kulegeza mikanda. Hatuna wazo lolote la kumvamia mtu ye yote; na wala hatutazamii kuvamiwa na mtu ye yote. Lakini ni vema kuwa tayari wakati wote kwa lolote linaloweza likatokea. Hilo ni funzo moja kubwa tulilopata kutokana na vita hivi.

Lazima jeshi letu liongeze sana uhodari wake. Lazima lijifunze kutokana na makosa, na vile vile kutokana na mafanikio, yaliyoonekana wakati wa vita. Wataalamu na maofisa wa jeshi letu lazima wajiendeleze kutokana na uzoefu waliopata vitani, na waongeze ujuzi wao zaidi. Na jambo la muhimu vile vile ni kwamba kwa kuwa sasa tumetambua umuhimu wa wanamgambo, basi lazima mafunzo yao yaimarishwe. Lazima wanamgambo wawe tayari wakati wote, kwa mazoezi na mafunzo ya mara kwa mara. Jeshi letu limejipatia sifa nzuri; si vema kuipoteza sifa hiyo.

Lakini kwa bahati mbaya ingawa vita vimekwisha, matokeo ya vita hivyo hayajesha. Hayo ndiyo yanayopaswa kushughulikiwa sasa, pamoja na matatizo mengine ambayo tulikuwa nayo kabla ya vita lakini tukayaweka kando wakati tulipolazimika kushughulika na vita vyenyewe.

Kundi la tembo linapoingia kijijini, wanakijiji huacha mambo yote na kujaribu kulifukuza kundi lile. Lakini watakapokwisha kulifukuza, na wanyama wale wakawa wameondoka, kazi yao huwa haijakamilika bado. Lazima watengeneze vilivyoharibika; lazima watengeneze nyumba zilizobomolewa, na kupanda upya mimea iliyovurugwa. Na bado itabidi waendelee kukabili matatizo waliyokuwa nayo kabla ya kushambuliwa na tembo.

Kadhalika na sisi. Lazima tutengeneze vilivyoharibika wakati wa vita. Lazima tujenge upya kila kitu katika Tarafa ya Missenyi, na kununua vifaa vilivyoondolewa visifanye kazi yake vikaenda kutumika vitani. Lazima tuwalipe askari na wanamgambo; na lazima tulipe fidia kwa wale waliouawa na kujeruhiwa, na vile vile tulipe gharama za kuwarudisha tena wananchi wa Missenyi katika vijiji vyao. Na kwa sababu ilitulazimu tukope ili tupate silaha kwa haraka wakati wa vita, sasa lazima tulipe madeni hayo.

Lakini si hivyo tu. Kwa kweli kutengeneza yaliyo-haribiwa na vita, au kulipa madeni ya vita, siyo kiini chote cha matatizo yetu ya sasa. Vita vimetuongezea tu matatizo hayo.

Tulikuwa na upungufu wa fedha za kigeni hata kabla hatujatumbukia katika vita mwezi Novemba, na moja ya sababu za upungufu huo ni kupanda kwa bei za mafuta ya petroli. Na mwaka huu uliopita umekuwa ni mwaka wa mvua nyingi mno. Mafuriko yameharibu sehemu kubwa ya barabara na madaraja katika mikoa mingi ya nchi yetu. Juu ya shida hiyo, bei ya mafuta tuliyolazimika kuyaagiza ilipanda kwa asilimia 40 zaidi.

Hatukuwa na uwezo wa kutawala mambo haya. Tuliposhambuliwa, tulilazimika kupigana. Mvua hatuku-zigimba sisi, wala hatukuwa na uwezo wa kuzisimamisha. Lakini madaraja yale hayapo tena, na kukosekana kwake kunasimamisha kazi ya kukusanya mazao kutoka vijijini, na kusafirisha bidhaa muhimu zinazohitajiwa vijijini. Lazima ipatikane njia ya kuyajenga madaraja hayo. Na wala hatuzungumzi habari ya daraja katika mto mmoja mkubwa, kama vile Kagera, ambapo tungeweza labda kuagiza daraja moja la dharura kutoka ng'ambo; haja sasa ni ya mamia ya madaraja madogo madogo ambayo ujenzi wake unahitaji saruji, au mawe, au vyuma na mafundi wengi na hodari.

Na bei ya mafuta hatuna uwezo nayo: wenye mafuta hutuambia bei, na kwetu sisi kilichobaki ni kukubali kuya-nunua kwa bei hiyo au kuyakosa. Lakini ni lazima tununue mafuta kama tunataka treni na malori yetu yasafiri,

kama tunataka viwanda vyetu au hospitali zetu zifanye kazi, na kadhalika. Na ni lazima tununue mafuta kwa fedha za kigeni, ambazo maana yake ni bidhaa tunazoziuza katika masoko ya dunia. Lakini bei ya pamba yetu na kahawa, na tumbaku, na korosho, na mazao yetu mengine tunayoyauza katika nchi za nje, hazijapanda. Kwa makadirio yetu ya sasa, itatubidi tutumie karibu nusu ya mapato yetu yote ya fedha za kigeni mwaka huu kununulia mafuta tu. Kwa hiyo tutakuwa na fedha za kigeni pungufu zaidi kununulia vifaa vingine tunavyovihitaji.

Kwa hiyo ni dhahiri kwamba tuna kipindi kigumu sana mbele yetu.

Hakuna njia ya kuiepuka shida hiyo. Lolote tutakalolifanya, na yako mambo tunayoweza kufanya, lazima tufahamu kuwa hali itakuwa ngumu sana katika Tanzania kwa kipindi cha miezi kumi na minane ijayo.

Baada ya kipindi hicho cha kadiri ya miezi kumi na minane hali inaweza ikaanza kuwa nzuri kidogo. Kwa hiyo kwa upande wa uchumi tumo katika hali ile ile kama tuliyokuwa nayo wakati wa vita. Hatuna budi tufanye mipango na tuanze kuitekeleza mipango hiyo kwa utaratibu, kabla hatujaanza kuona matokeo yo yote. Lakini ingawa matayarisho ya kuvuka mto na kuanza kumpiga adui yalichukua majuma machache tu, itachukua muda mrefu zaidi kabla uchumi wetu haujaanza kuimarika.

Tumekwisha kuanza mipango na matayarisho; kwa kweli yamekuwa yakiendelea kwa muda mrefu, maana sehemu kubwa ni maendelezo ya mipango yetu ya kawaida ya maendeleo. Viwanda vingi sasa vimo katika kujengwa, pamoja na viwanda vipya viwili vya saruji. Mkataba mmoja muhimu wa kuchimba madini umekwisha kutiwa sahihi, na mingine imo katika majadiliano. Lakini mambo yote haya huchukua muda. Unaweka jiwe la msingi la kiwanda mwaka huu, halafu miaka mingi inapita kabla kiwanda hicho hakijaanza kutoa bidhaa. Baada ya kugundua madini, na sasa tunajua ya kwamba tunayo madini, ni lazima uwe mwangalifu sana katika majadiliano ya mikataba ya kuyachimba madini hayo. Hatuwezi kukubali kuuza

nchi yetu, hata katika kipindi hiki kigumu. Na halafu inatakiwa utumbukize fedha nyingi, na ungoje muda mrefu, kabla hujaanza kuyauza madini hayo na kupata fedha za kigeni, au kuyatumia badala ya kuagiza madini kama hayo kutoka nchi za nje.

Kwa hiyo tunajua kwamba hali itakuwa nzuri. Lakini kwanza lazima tuvuke kipindi kirefu cha shida.

Hatutakuwa na shida ya chakula; chakula kitakuwako tele kwa watu wote. Lakini hatutaweza kuchagua chakula tutakacho siku zote. Mpunga uliharibiwa na mafuriko huko Kyela, Rufiji na Kilombero, na katika sehemu nyingine linakolimwa zao hilo. Kwa hiyo katika msimu huu mpunga tuliovuna si mwingi sana. Tunatazamia kupata mchele kidogo na ngano kutoka nje. Lakini inafaa tutambue kwamba hatuna fedha za kigeni za kuagizia mchele mwingi au ngano kutoka nje. Lakini vyakula vingine tunavyo kwa wingi. Hakuna sababu ya mtu ye yote kufa kwa njaa au kudhoofika kwa ukosefu wa chakula.

Tutakuwa na upungufu wa vitu vingine vingi ambavyo tungependa tuvipate kutoka nje kama tungekuwa na fedha za kigeni. Lakini fedha hatuna kwa hiyo hatuwezi kuvinunua. Mtanzania anafahamu tatizo hilo katika maisha ya nyumbani mwake mwenyewe. Na kwa nchi ni vivyo hivyo. Tutatumia fedha kidogo za kigeni tulizonazo kununua vitu vile tu ambavyo ni muhimu kabisa. Kutakuwako usimamizi mkali juu ya umuhimu wa vitu na tutagawa fedha zetu za kigeni kufuatana na mpango huo. Tutatoa umuhimu wa kwanza kwa vifaa vitakavyotusaidia kutoa bidhaa muhimu, na vile vitakavyotuwezesha kupata fedha za kigeni zaidi. Vitu vya matumizi ya kawaida vitakuwa chini kabisa katika umuhimu huo.

Na kwa sababu hatutaweza kununua malori mapya, mabasi, mabehewa, na injini za treni zote tunazozihitaji, wala hatutaweza kununua vifaa vya kutengenezea madaraja na mabarabara yetu yote yanayohitaji kutengenezwa, ni dhahiri kwamba matatizo ya usafiri yataendelea. Matatizo hayo yatafanya shida iliyoko sasa ya kusambaza bidhaa vijijini kuwa kubwa zaidi.

Nawaelezeni mambo haya bila kificho, kwa sababu sitaki tujidanganye. Matatizo yetu ni makubwa na yataendelea kwa muda mlefu. Katika kuyakabili, kama vile wakati wa kukabili matatizo ya vita, hatuna budi tushirikiane vizuri sana. Ifanyeni hatari ya matatizo haya kuwa ni sawa sawa na hatari ya uvamizi wa Amin.

Lakini hata katika kuikabili hatari hii uwezo tunao. Kama tukishirikiana vizuri tutaweza kulishinda tatizo hili la uchumi kama vile tulivyolishinda lile la uvamizi. Bora tu kila mmoja wetu atimize wajibu wake hapo alipo.

Kwanza hatuna budi kuongeza utoaji wa mali. Hatuna budi kuongeza mazao ya kila aina. Hili zaidi ni jukumu la wananchi wa vijijini; wakulima. Lakini wananchi wanaoishi mijini yawapasa pia wajitahidi kupanda cho chote wanachoweza kulima kwa chakula chao. Mradi tu wasivunje kanuni za usafi wa miji yao. Vile vile lazima tuzidishe mazao yetu ya kuuza nchi za nje: pamba zaidi, kahawa, korosho, tumbaku, mkonge, na kadhalika. Kiasi kinachopatikana cha baadhi ya mazao hayo kimekuwa kikipungua; hatuna budi tukiongeze, tena kwa haraka.

Hatuna budi vile vile tufanye kazi kwa ufanisi zaidi katika viwanda vyetu na katika ofisi zetu, na katika kazi za usafirishaji. Tuache kabisa uzembe. Watu wasiotaka kutimiza kazi yao ya kutwa lazima waondolewe na wawekwe wengine ambao watakuwa tayari kufanya kazi ya haki kulingana na ujira wao. Na mameneja wetu ndio wanaopaswa kuonyesha mfano. Kazi zao zitakuwa ngumu zaidi kuliko ilivyo kawaida, kwa sababu ya matatizo ya fedha za kigeni. Lakini kama vitaagizwa vifaa vichache, muhimu, na kama kuagiza huko kutafanywa mapema na kama wanaohusika na kuagiza huko watajishughulisha kuvifuatia, basi matatizo yanaweza kuepukwa, kupunguzwa, au kuondoka kabisa. Katika vita hivi vya kupambana na matatizo yetu ya uchumi, meneja mbovu ni mtu wa hatari zaidi kuliko mfanya kazi mzembe. Na yeye ni vizuri aondolewe ili mahali pake pashikwe na meneja mwenye uwezo zaidi.

Kutoa mali ni jambo la lazima. Lakini kutunza vifaa tulivyonavyo, na kuzuia uharibifu, ni jambo la lazima vile vile. Wafanyakazi wetu wote, na kwa kweli wananchi wote, wana wajibu mkubwa katika suala hili.

Lazima magari yatengenezwe vizuri, na kwa uangalifu. Lazima yatiwe mafuta wakati wake, na lazima yaendeshwe kwa uangalifu. Baadhi ya madereva wetu wa mabasi, na malori huendesha magari yao kana kwamba kuna mashindano. Huzidisha mwendo uliokadiriwa kwa magari yao, na kwa hiyo hutumia petroli zaidi kuliko ambavyo wangetumia kama wangekwenda mwendo wa kadiri. Na wanakwenda katika kona kwa mwendo wa kasi mno, hata wakati mwingine magari yao hupinduka mahali pazuri kabisa. Na kila gari linalopinduka maana yake ni uharibifu: uharibifu mkubwa wa fedha za kigeni, na mara nyingi uharibifu wa maisha ya Mtanzania pia.

Haja ya kutunza vifaa iko kila mahali: katika viwanda, hospitalini, na katika ofisi. Hata katika mashamba yetu kuna vifaa kama maplau, mapanga, haro, n.k. ambavyo vinahitaji matunzo, bila kuhesabu matrekta na mikokoteni ambayo wakati mwingine husahauliwa mahali mpaka ikaoza!

Na hatuna budi kuchukua hatua maalum kuondoa uharibifu wa vifaa. Kuna mtu aliyesema, "Gurudumu la Serikali ni karatasi". Lakini tunatumia karatasi nyingi mno. Mimi naamini ya kwamba tungeweza kutumia karatasi kidogo zaidi katika Serikali ya Tanzania, na pengine kubakiza akiba ya kuweza kutumiwa shuleni ambako kuna upungufu mkubwa zaidi. Siku moja niliona taarifa ya mistari miwili iliyotoka katika ofisi moja ya Ikulu kwenda katika ofisi nyingine ya Ikulu. Karatasi nzima na bahasha mbili zilitumika kwa sababu hiyo. Na makaratasi haya tunayanunua kutoka katika nchi za nje kwa fedha za kigeni!

Na zaidi ya yote lazima tuwe waangalifu sana katika matumizi ya mafuta: ya petroli, dizeli, na mafuta ya taa. Serikali imekwisha kutangaza hatua fulani za kupunguza matumizi ya mafuta kwa magari ya umma. Lakini Serikali hutoa mwongozo tu: wanaotekeleza ni wananchi.

Na suala hili kwa kweli linawahusu maofisa na wananchi wanaoishi mijini. Wananchi wa vijijini huenda mashambani kwao kwa miguu; au katika maeneo yenye watu wengi, mtu huenda kutembea kijiji cha pili kwa miguu. Pengine na sisi, inapokuwa si lazima tutumie chombo cha mafuta, ingefaa tuige mfano wa wanavijiji.

Narudia tena. Kipindi cha miezi kumi na minane ijayo kitakuwa kipindi kigumu sana kwa kila mwananchi. Chama na Serikali vinanuia kuusawazisha mzigo huo ili kila mmoja wetu aubebe kwa haki kadiri itakavyowezekana. Tutayachunguza mambo hayo kwa undani zaidi katika majuma machache yajayo. Lakini kila mmoja wetu, atabeba sehemu yake ya mzigo huo; hakuna atakayesamehewa. Hatuna njia ya kuepukana na tatizo hilo.

Lakini mimi nina imani. Tumekwisha kushinda vita ambavyo ni watu wachache tu nje ya nchi hii waliamini kuwa tutaviweza. Tumeshinda kwa sababu ya umoja wetu, ari yetu, na nidhamu yetu. Kwa silaha hizo hizo juhudi yetu itashinda matatizo ya uchumi.

Mashujaa wetu tunaowapongeza leo wametuonyesha mfano na wametutia moyo. Tunawakaribisha tushirikiane katika mapambano haya mapya.

Mapambano yanaendelea.